

# Pamoja Kuelekea Njia ya Msalaba

## Juma Takatifu

6-12 Aprili 2020

FUNGAMANO
LA MAKANISA
YA KILUTHERI
DUNIANI

# Utangulizi

Majira ya Mateso ni wakati wa kujikagua, kuomba, kufunga, na kushirikishana vipawa vya neema. Wakati waumini wengi wakianzisha safari yao ya kuamshwa upya kiroho, maisha ya Kikristo yanaenda mbali zaidi ya juhudi binafsi za mtu mmoja mmoja. Hija yetu duniani ni ya mtu mmoja mmoja, ya ushirika na ya kiulimwengu pia. Inahusu maisha yetu pamoja, na wito wa kutiana moyo sisi kwa sisi katika nyakati hizi za majaribu mengi.

Tunatoa muongozo huu kuwaongoza waumini wenzetu katika kukiri 'umoja' ndani ya ushirika wa Makanisa ya Kilutheri katika dunia nzima. Mpangilio wake uko katika sehemu tatu kwa kufuata muongozo wa Luther wa kufanya theologia kwa njia ya sala (oratio), tafakuri (meditatio), na kujaribu/kupambana (Tentatio). Majira haya hasa, yanatoa fursa ya sisi wenyewe kuzama ndani ya dunia ambako:

> kuna kujaribu/kukata rufaa (tentatio). Hiki ni kipimo. Kinatufundisha si tu kujua na kuelewa bali pia kuona jinsi kwa njia ya Neno la Mungu, haki, ukweli, uzuri, kupendeza, nguvu na kufariji vilivyo: Ni hekima ya juu kabisa (Martin Luther, Luther's Works: Career of the Reformer. Vol. 34, 286-87.)

Tukiwa tumesukumwa na Luther, tunatakiwa tujenge utamaduni wa kuomba na kutafakari pamoja kama ushirika wa Kristo. Tunapotambua hekima ya Mungu kwa njia ya mapambano yenye masumbufu mengi katika dunia yetu ya leo, mara nyingi tukiwa tumejeruhiwa na kuharibiwa na migawanyiko, kukata tamaa na kutoweka kwa matumaini, imani yetu inatupa matumaini mapya tukivumilia na kutembea pamoja bila kujali mambo yetu.

Hakika, Mungu hutembea na kila mmoja wetu hatua kwa hatua kwa njia ya msalaba.

Kumbuka: Maombi yote yamenukuliwa kutoka *Koinonia: Services and Prayers* (Geneva: The Lutheran World Federation, 2004). Mistari yote ya Biblia ni kutoka Maandiko Matakatifu ya Mungu Yaitwayo Biblia Yaani Agano la Kale na Agano Jipya.

# Jumatatu, 6 Aprili 2020

## Tuombe Pamoja

Mungu mwenye huruma, utupe sisi mioyo yenye shukrani,
kwa ajili ya haya yote na vipawa vyako vingi,
na utupe kufikiri juu ya mahitaji ya wengine,
kwa njia ya Yesu Kristo, Mwokozi na Bwana wetu. Amen

## Tutafakari Pamoja

Isaya 42:1-9
Waebrania 9:11-15
**Yohana 12:1-11**

7 Basi Yesu alisema, Mwache aiweke kwa siku ya maziko yangu. 8 Kwa maana maskini mnao siku zote pamoja nanyi; mimi hamnami siku zote.

## Tutembee pamoja

Tunawashukuru wanawake ambao wanatusaidia kutambua umuhimu wa uwepo wa Kristo katikati yetu. Amen

# Jumanne, 7 Aprili 2020

## Tuombe Pamoja

Tuma malaika wako,
kutuongoza katika njia yetu
ili turudi nyumbani kwetu
tukiwa na afya, usalama na furaha. Amen

## Tutafakari Pamoja

Isaya 49:1-7
1 Wakorintho1:18-31
**Yohana 12:20-36**

35 Basi Yesu akawaambia, Nuru ingaliko pamoja muda kidogo. Enendeni maadamu mnayo
nuru hiyo, giza lisije likawaweza; maana aendaye gizani hajui aendako. 36 Maadamu mnayo
nuru, iaminini nuru hiyo, ili mpate kuwa wana wa nuru.

## Tutembee Pamoja

Tuzipinge nguvu za giza zinazolenga kutupita na kutupoteza, badala yake tuulenge mwanga unaotoa mwongozo kuelekea kwenye 'uzima', 'usalama' na 'furaha'. Amen.

# Jumatano, 8 Aprili 2020

## Tuombe Pamoja

Ee Mungu, umeumba mbingu na nchi,
***tuangalie sisi.***

Ee Mungu, unatukumbatia watu wako,
***tuepushe na mabaya.***

Ee Mungu, unatulinda tuingiapo na kutoka,
***tubariki sisi sasa na hata milele. Amen***

## Tutafakari Pamoja

Isaya 50:4-9a
Waebrania 12:1-3
**Yohana 13:21-32**

21 Naye alipokwisha kusema hayo, Yesu alifadhaika rohoni, akashuhudia akisema, Amin,
amin, nawaambieni, Mmoja wenu atanisaliti.

## Tutembee Pamoja

Mioyo yetu isifanywe migumu na hali tuliyoizoea ya usaliti; lakini badala yake hebu tupate nguvu kutoka kwake anayeelewa kikamilifu udanganyifu wa moyo wa mwanadamu. Amen.

# Alhamisi Kuu, 9 Aprili 2020

## Tuombe Pamoja

Ee, Mungu mwenye neema,
ulitupa Ushirika Mtakatifu kama chakula cha upendo,
na kwa kuwaosha miguu wanafunzi,
Mwana wako, alituelekeza sisi maisha ya huduma inayotakiwa,
Utupe maisha na nguvu kwa njia ya fumbo la sadaka hii,
kwa njia ya Yesu Kristo, Mwokozi na Bwana wetu. Amen

## Tutafakari Pamoja

Kutoka 12:1-4, (5-10), 11-14
1 Wakorintho 11:23-26
**Yohana 13:1-17, 31b-35**

14 Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo
hivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi.
15 Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi
nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo.

## Tutembee Pamoja

Tunatamani kwenda mbali zaidi ya alama ya tendo na badala yake tuhudumu katika njia zilizowazi, tukihakikisha kuwa utumishi ulio sawa na Kristo umevalishwa kwa dhati katika maisha yetu ya pamoja na huduma kwa wote. Amen.

# Ijumaa Kuu, 10 Aprili 2020

## Tuombe Pamoja

Mungu Mwenyezi na uishiye Milele,
kwa upendo wako mwororo
umemtuma kwetu Mwana wako, Bwana wetu Yesu Kristo
kuchukua kutoka kwetu asili yetu,
na kuteseka hadi kufa pale msalabani.
Tujalie kutembea katika njia ya mateso yake
na kushirikishana furaha ya ufufuko wake,
kwa ajili ya Yesu Kristo, Mwokozi na Bwana wetu. Amen.

## Tutafakari Pamoja

Isaya 52:13-53:12
Waebrania 10:16-25 au Waebrania 4:14-16; 5:7-9
**Yohana 18:1-19:42**

37 Basi Pilato akamwambia, Wewe u mfalme basi? Yesu akajibu, Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu.
38 Pilato akamwambia, Kweli ni nini?

## Tutembee Pamoja

Katika dunia iliyotawaliwa na uongo na udanganyifu, ni lazima tufuate njia ya msalaba ambayo huisitiri kweli hata kama itaalika tufanyiwe dhihaka na mateso. Amen.

# Jumamosi Takatifu, 11 Aprili 2020

## Tuombe Pamoja

Laiti ungenificha kuzimuni,
Ukanilinda kwa siri, hata ghadhabu zako zitakapopita,
Na kuniandikia muda ulioamriwa, na kunikumbuka!
Mtu akifa, je? Atakuwa hai tena?
Mimi ningenjoja siku zote za vita vyangu,
Hata kufunguliwa kwangu kunifikilie.
– *Ayubu 14:13-14*

## Tutafakari Pamoja

1 Petro 4:1-8
**Yohana 19:38-42**

40 Basi wakautwaa mwili wake Yesu, wakaufunga sanda ya kitani pamoja na yale manukato,
kama ilivyo desturi ya Wayahudi katika kuzika.

## Tutembee Pamoja

Tuambatane na wale wote waliolemewa na hofu, lakini bado wanafanya yale yaliyo ya haki na mema nyuma ya pazia pasipo kuonekana na umma. Amen.

# Jumapili ya Pasaka, 12 Aprili 2020

## Tuombe Pamoja

Mungu uliye mwema katika yote,
kwa njia ya ufufuo wa Mwana wako Yesu Kristo
asubuhi ya upya wa uumbaji wake imepambazuka,
Siku aliyoifanya Bwana imewadia,
visima vya wokovu vimefunuka.
Katika Ubatizo Mtakatifu umeungana nasi
katika maandamano ya ushindi wa Kristo.
Utupe sisi wote roho ya ufufuo,
ili tukutukuze wewe milele
na kufurahi katika kipawa hiki cha wokovu,
kwa ajili ya Yesu Kristo Bwana wetu,
aishiye na kumiliki pamoja nawe na Roho Mtakatifu,
Mungu mmoja, milele hata milele. Amen

## Tutafakari Pamoja

Yohana 20:1-18
Yeremia 31:1-6
**Matendo 10:34-43**

39 Nasi tu mashahidi wa mambo yote aliyoyatenda katika nchi ya Wayahudi na katika
Yerusalemu; ambaye walimwua wakamtundika mtini. 40 Huyu Mungu alimfufua siku ya tatu,
akamjalia kudhihirika, 41 si kwa watu wote, bali kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha ku-
chaguliwa na Mungu, ndio sisi, tuliokula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka kwake
kutoka kwa wafu.

Yesu ni Bwana wa wote! Ujumbe wa amani tayari ulianza „baada ya ubatizo uliotangazwa na Yohana.“ Mungu alimweka wakfu Yesu kwa njia ya Roho Mtakatifu na kwa uweza (Matendo 10). Ujumbe huu wa amani - ujumbe wa Pasaka - tayari unaweza kujidhihirisha katika maisha ya Yesu, akifanya mema na kuponya wale wote waliokandamizwa

na uovu. Ufufuo ni kazi ya Mungu inayoendelea, ambamo watu wote waliobatizwa wanashughulishwa. Tumeitwa kuponya wale wote wanaokandamizwa na nguvu na mamlaka - ambazo zinapingana na Mungu na ambazo zinawatenga wanadamu na Mungu na kati ya wao kwa wao. Ufufuo unavunja milango ya gereza na kuiacha wazi, unaondoa vikwazo, unavunja kuta, na kutuokoa kutoka mambo yote yaliyotufunga na kutukandamiza na kutugawa kwa misingi ya kibinafsi, ki makundi ya watu, kimataifa na kutugawa wenyewe kwa wenyewe.

Tangazo la Ufufuo linatuingiza kuelekea tendo la Mungu, ndani ya mpango wa Mungu ambao Mungu anaendelea kuukamilisha, akishinda kifo katika hali zake nyingi na kutualika wote kwenye jumuia iliyopatanishwa. Fumbo hili la kuirudisha na kuipatanisha dunia na Mungu mwenyewe limedhihirishwa na Mungu kwa wale ambao ni „mashahidi," kwa wale walio kula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka kutoka kwa watu (Matendo 10), kwa wale walioshiriki chakula pamoja naye. Chakula cha uumbaji mpya ni meza ya mwaliko pia. Bwana Mfufuka anasubiri na kuita. Wote na waje wachukue wema wa Mungu unaopenya dunia nzima. Chakula tu chenyewe kinaondoa vikwazo. Katika karamu hii, Mungu anatambuliwa.

Haleluya Kristo Amefufuka! Kristo amefufuka kweli kweli Haleluya!

## Tutembee Pamoja

Hatujaitwa kuhukumu bali kuwa mashahidi waaminifu „tunaokiri kwamba Kristo ndiye mmoja aliyebarikiwa na Mungu kuwa hakimu wa wanaoishi na waliokufa." Amen.